TOLEO NO.72

# Khilafah

RAMADHANI 1447 HIJIRIA —MACHI 2026 MILADIA ( Bei Tsh 4,000/= - Ksh 200/=)

NDIO SULUHISHO

## TAREHE 03 MACHI SIKU YA MSIBA MZITO KWA KUANGUSHWA DOLA YA KHILAFAH



Dola ya Kiislamu ya Khilafah iliyokuwa muendelezo wa dola aliyoiasisi Mtume SAAW iliangushwa rasmi tarehe 03/03/1924 / 27 Rajab1342. Dola ambayo ilidiriki kuzishinda tawala za Uajemi na Warumi (Byzantine) na kubakia kuwa dola kuu mpaka karne ya 18. Makafiri waliweza kuiangusha kufuatia kudhoofika kifikra, kuzongwa na maadui wa ndani na nje pia kampeni kabambe ya madola ya kibepari ndani ya Ulaya na Marekani. Khilafah ilikuwa ikisimamia hukmu za Kiislamu, kuwaunganisha Waislamu, kufunguwa miji nk.

Mara baada ya kuangushwa dola hiyo kulifuatiwa na hali isiyosita ya udhalilifu, majanga na maafa yasiyomithilika kwa Ummah wa Kiislamu kwa kuvamiwa, kuteswa, kuuwawa, kuchukuliwa nchi zao, kusambaratishwa uhai wa umoja wake, kugawanywa kimadhehebu na kitaifa taifa kiasi cha kukosa sauti moja yenye athari katika anga za kimataifa nk.

Majanga yote leo yanayotusibu kitaifa, kieneo na kimataifa ni matokeo ya kukosa kinga (dola) ya kuwanusuru Waislamu na kudhamini maisha, heshima na usalama wao. Tunashuhudia kwa macho mawili uvamizi wa makafiri katika miji yetu kama Gaza, Iran,Lebanon Sudan nk. Aidha, kumeshamiri dhulma kama mateso na ubaguzi wa kidini kama ndani ya Kashmiri, Mymanar, Turkistan mashariki nk.

Kuvunjwa Khilafah ni mpango kabambe wa nchi za kikafiri za ki-Magharibi kwa ajili ya kuendeleza sera zao za kigeni, kuuvuruga mfumo wa Kiislamu, kunyakuwa rasilmali zake na kumakinisha mfumo wao batil wa kibepari. Kufikia malengo hayo walitumia mikakati mbalimbali ikiwemo vibaraka kama Sharrif Hussein, Kamal Atarturk, Ibn Saud nk. Pia kuunga mkono harakati za kujitenga kwa maeneo yaliokuwa chini ya Khilafah kwa jina la

**Inaendelea Uk. 3**

## DIKTETA TRUMP NA KITIMBAKWIRI WAKE DOLA YA KIYAHUDI WAZINDUA MASHAMBULIZI MAKUBWA DHIDI YA IRAN



Marekani na dola ya Kiyahudi zimeanzisha mashambulizi ya pamoja na mapana dhidi ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran leo Jumamosi, huku milipuko mikubwa ikisikika katika mji mkuu wa Tehran na miji kadhaa ikiwemo Qom, Isfahan, Kermanshah na Karaj.

Rais wa Marekani, Donald Trump, alitangaza kuanza kwa operesheni hiyo ya kijeshi akisema: “Dakika chache zilizopita tumeanza operesheni kubwa za kijeshi nchini Iran.” Kituo cha 12 cha televisheni cha Israel kiliripoti kuwa Israel imelenga makumi ya shabaha zinazohusishwa na taasisi za serikali ya Iran (Al Jazeera, 28/02/2026).

Kauli za Trump ziliambatana na tambo na majigambo, akidai kuwa Marekani na jeshi lake ndilo lenye nguvu zaidi duniani, na kwamba hatairuhusu

**Inaendelea Uk. 5**

## Yaliyomo :


- **Kuvunjwa Khilafah: tumekosa Amiri jeshi wa kweli ……..…..2**
- **Wanawake wa Kiislamu mna ujira mkubwa…………………...4**
- **Kuuzwa akiba ya dhahabu ya Tanzania ……………………..6**

## KUVUNJWA KHILAFAH: TUMEKOSA AMIRI JESHI WA KWELI

Tumeingia mwaka wa 102 tangu makafiri wakiongozwa na Uingereza kuiangusha Khilafah ya mwisho mnamo tarehe 3 Machi 1924. Hilo lilifanikiwa kutokana na usaliti na khiyana ya vibaraka katika waturuki na waarabu.

Matokeo ya tukio hilo ni Umma wetu kusibiwa na kila aina ya balaa na majanga. Kuanzia vita, umasikini, ujinga, dhulma, mateso kutoka kwa makafiri na vibaraka wao katika ulimwengu wa Kiislamu na penginepo.

Si hayo tu, bali ardhi za Waislamu zimekatwa vipande vipande, na Umma wetu ukasambaritishwa kwa jina la mipaka ya kijografia iliyochorwa na makafiri kwa maslahi yao.

Kumbukumbu ya kuangushwa Khilafah mwaka huu inaambatana na Ramadhani, bali pia inaambatana na vita kutoka kwa makafiri dhidi ya Umma wetu na biladi zetu. Yaani mashambulizi ya Marekani na wakala wake kijidola bandia cha Israel tangu tarehe 28 Februari 2027/ 11 Ramadhani 1447 Hijria ndani ya Iran ambapo wanaendelea kudamirisha roho za Waislamu, mali, miundo mbinu nk. Allah Taala Awanusuru Waislamu na Awangamize makafiri hawa. amiin.

Makafiri hawa kamwe hawatoheshimu dini, ubinadamu wala murua, ndio maana kwa makusudi wanaasisi vita ndani ya mwezi wa Ramadhani wakilenga kuudhalilisha Umma. Na kwa hakika hivi sio vita vya mwanzo kuasisiwa na makafiri wa kibepari ndani ya Ramadhani. Kuna vita vya 'Harb Ramadhan' dhidi ya Israel mwaka 1973, vita vya Marekani vya Ghuba vya pili nk.

Wakati tukitaja vita hivyo vilivyoasisiwa na makafiri wa kibepari ndani ya Ramadhani kwa makusudi, haina maana kwamba Waislamu wanaogopa kupigana ndani ya Ramadhani, la hasha! Kuna vita vingi Waislamu walipigana ndani ya Ramadhani kwa ari, ujasiri na kuibuka na ushindi mnono mkubwa. Vita kama vya Badr, Fathi Makka, Ain Jaloot, Fathi ya Andalusia nk. vyote vilipiganwa ndani ya Ramadhani. Kwa hivyo, vita ndani ya Ramadhani halijawahi kuwa tatizo kwa Umma, bali suala mbele yetu, katika hali ya leo Waislamu tunapigana tukiwa vipi?

Naam, vita tunavyopigana Waislamu leo dhidi ya makafiri iwe Ramadhani au muda mwingine vinapiganwa ilhali tukiwa hatuna sauti moja, bendera moja na msimamo mmoja. Hilo ni kwa sababu hatupo chini ya kiongozi mmoja yaani Khalifah. Pamoja na ukweli kuwa Waislamu huwajibishwa na sharia kupigana wanapovamiwa pawe na Khalifah au la, lakini lau angekuwepo Khalifah hali na matokeo yangekua tofauti.

Leo Waislamu wanapigana katika hali ambayo licha ya kuwa wanapambana dhidi ya makafiri, lakini kambi, vituo vya kufanyia

mashambulizi na maficho ya makafiri hao ni katika ardhi zetu. Kama tulivyoona awali katika vita viwili vya Ghuba na mashambulizi haya yanayoendelea. Majeshi ya Marekani yanapanga, kuratibu na kuendesha mashambulizi yao kutoka katika biladi za Waislamu, iwe Qatar, Saudia, Bahrain, Kuwait, Falme za Kiarabu nk. Jambo hili ni zaidi ya aibu. Kafiri Marekani na myahudi wanawapiga na kuwadhuru Waislamu kwa kutumia ardhi za biladi zetu !!

Aidha, Waislamu wanapigana leo vita dhidi ya makafiri ilhali tukiwa tumegaiwa na makafiri kwa mipaka ya kijografia, kiasi cha baadhi ya Waislamu kuona kwamba mashambulizi yanayofanywa na makafiri katika biladi ya Waislamu hauwahusu wao, bali unawahusu eneo palipofanywa uvamizi.

Mwisho, Waislamu wanapigana vita na makafiri leo ambapo wapiganaji wengi kama sio wote huwa na ikhlasi, lakini baadhi ya wanasiasa nyuma yao huwa wakala wa makafiri ambapo mwisho hudhoofisha jitihada yao, huuza misimamo au kutiliana makubaliano ya kikhaini na makafiri. Mfano, Sadaat, Al-Jaulani nk.

Kumbukumbu ya kuangushwa Khilafah itusukume kufanya kazi ya kurejesha tena dola hiyo, ili Umma wetu upate kiongozi thabiti, mkweli, mchaMungu anaepaswa kuziunganisha biladi za Waislamu na kuwa amiri jeshi wa jihadi kwa Umma wetu.

**Mhariri**

**Ramadhani 1447 Hijria**

**Machi 2026 M**

***jukwalakhilafah@gmail.com***

************

## Kuangushwa Dola ya Khilafah ... *kutoka uk .1*

'uhuru' ili kuimega mamlaka ya Khilafah. Itakumbukwa pia Uingereza, Ufaransa na Urusi zilikubaliana mkataba wa siri wa Sykes-Picot Agreement ili kugawana ardhi za dola ya Khilafah.

Katika Vita Vikuu vya Kwanza malengo ya kuivunja Khilafaha yalikwenda kwa haraka zaidi. Nchi washirika baada ya kushinda zilinyakua maeneo muhimu ya Khilafah. Chini ya uongozi wa Uingereza zilimlazimisha Khalifah, kiongozi wa dola ya Kiislamu kusaini mkataba hapo tarehe 30 Oktoba 1918 ulioitwa wa amani ukiwa na lengo la kuipunguza nguvu dola hiyo.

Uingereza kwa kushirikiana na kibaraka wake Yahudi muovu na msaliti Mustafa Kamal aliyekuwa kamanda wa kijeshi wa Uturuki walianzisha uasi dhidi ya Khilafah. Mnamo tarehe 1 Machi 1924 Mustafa Kamal alitoa agizo bungeni la kuvunjwa Khilafah na asubuhi ya tarehe 3 Machi 1924 ilitangazwa rasmi kuvunjwa dola hiyo na kutenganishwa dini mbali na serikali. Mkataba wa Lausanne (Lausanne Treaty) ukasainiwa tarehe 24 Julai 1924 ukifuatiwa na kutambuliwa rasmi uhuru wa Uturuki. Uingereza ilitoa zawadi kwa makubaliano na Mustafa Kamal kujiondoa katika maeneo yote iliyoyakalia ya Uturuki na kuutambua rasmi uhuru wa dola hiyo. Mmoja wa wabunge ndani ya Bunge la Uingereza alipinga hatua ya nchi yake kutambua uhuru wa Uturuki. Waziri wa Mambo ya Nje wa Uingereza Lord Curzon alifafanua na kumliwaza mbunge huyo kwa kumjibu bungeni :*"Suala ni kwamba Uturuki imeshabomolewa na haitokuja juu tena, kwa kuwa tumevunja nguvu yake ya kiroho: Khilafah na Uislamu."*

**Enyi Waislamu,**

Hivi ndivyo dola yenu tukufu ya Khilafah ilivyoangushwa, na majanga ya kuangushwa kwake yapo mbele ya macho yenu waziwazi kitaifa na kimataifa.

Basi shime tubebeni jukumu la kuirejesha kwa ikhlasi kuikimbilia bishara ya Mtume SAAW ya kurejea tena kwa dola hiyo yenye nuru na neema kwa wanadamu wote

ثم تعود خلافة على منهاج النبوة..

***….'.Kisha itarudi tena Khilafah kwa njia (manhaj) ya Utume'***

**************




## MATUKIO YA MACHI

3-03- 1924 Kuangushwa Khilafah ya Mwisho

3-03 Siku ya Kimataifa ya Wanyamapori (World Wildlife Day)
8-03 Siku ya Kimataifa ya Wanawake
Kila Jumatatu ya pili ya Machi - Siku ya Jumuiya ya Madola (Commonwealth Day) http://www.royal.gov.uk/MonarchAndCommonwealth/QueenandCommonwealth/CommonwealthDay.aspx

20-03- 2003 -Uvamizi wa Marekani ndani ya Iraq

21-03 Siku ya Mama Duniani (Mother'sday)

21-03 Siku ya Kimataifa ya Kukomesha Ubaguzi

21-03 -1961 Kumbukumbu ya Mauwaji ya Kikatili ya Sherpervile (Afrika ya Kusini)

22-03 Siku ya Kimataifa ya Maji (World Water Day)

23-03 Siku ya Kimataifa ya Hali ya Hewa

24-03 Siku ya Kimataifa ya Kifua Kikuu

25-03 Siku ya Kimataifa kuwakumbuka wahanga wa utumwa na biashara ya Utumwa kupitia bahari ya Atlantiki (Transatlantic Slave Trade)

## UPASUAJI KWA AJILI YA MAPAMBO

**Swali:**

Ni ipi Hukmu ya Kishari'ah Juu ya Upasuaji wa mapambo/ kufanya oparesheni kwa ajili ya mapambo,

**Jibu:**

**Kwanza**: Ikiwa sababu ya upasuaji huo ni kwa ajili ya matibabu, kwa mfano kufanya upasuaji ili urekebishe sehemu ya mwili iliyosababishwa kuharibika, mfano na maradhi, ajali au kuchomeka, au kurekebisha kasoro za kuzaliwa kama kumkata mtu aliyezaliwa kidole kilichozidi urefu au kuvitenganisha vidole vilivyoshikana na mfano wa haya. Upasuaji aina hiyo unaruhusiwa na ushahidi wa hilo ni alivyosimulia al-Tirmidhi kutoka Arfajah ibn As'ad alisema:

***"Pua yangu ilikuwa imekatika vibaya Siku ya Al-Kulab wakati wa Ujahiliya. Kwa hiyo nikatumia pua ya Wariq (shaba) ambayo ilikuwa inaisha polepole, hivyo Mtume (saw) akaniagiza nitafute mfano wa pua iliyotengezwa kwa dhahabu"***

**Maana ya "pua ya Wariq" ni ya shaba. Hii inaashiria kuwa upasuaji wa plastiki (plastic surgery) kwa ajili ya matibabu inaruhusiwa.**

**Pili:** Ikiwa upasuaji huo ni kwa ajili ya kuboresha muonekano ili kuvutia kimuonekano na sio wa matibabu basi hauruhusiwi

**uk..7**

## WANAWAKE MNA UJIRA MKUBWA

Suala la malipo kwa mwanadamu ni suala ambalo halina shaka kwa mwenye imani thabiti mbele ya Mola wake. Lakini kuna suala la kujiuliza hasa kwa akinamama na madada zetu kwa kuwa wao muda mwingi huwa na majukumu ya ndani ya nyumba zao tofauti na waume zao.

Aidha, inadhihirika kuwa wanaume hupata muda mwingi zaidi wa kufanya ibada ziada jambo alinaloweza kuleta hisia kuwa watapata darja kubwa mbele ya Allah Subhanahu Wataala. Ilhali wanawake wakaona, wao ni wenye nafasi ndogo tofauti na darja kama za waume zao au makaka zao.

Asma bint Yazid al-Answari (r.a) anatuelezea juu ya suala hilo. Siku moja alikwenda kwa Rasulullah Sallallahu Alaihi Wasallam na akamwabia:

*"Ewe, Rasullullah! Wewe ni kipenzi kwangu mimi kuliko wazazi wangu. Wanawake wa Kiislamu wamenituma kama mwakilishi wao ili nije nizungumze nawe kwa niaba yao. Bila shaka wewe ni Rasulullah kwa wanawake na wanaume pia. Sisi hupitisha wakati wetu zaidi baina ya kuta nne za majumba yetu. Tumefungika katika wajibu wetu wa kutosheleza shahawa za waume zetu, kuwazalia watoto na kuwatunzia majumba yao. Licha ya haya yote, wanaume wanatushinda katika kupata thawabu kwa mambo ambayo sisi hatuwezi kuyafanya. Waohuenda msikitini wakaswali swala zao kwa jamaa kila siku, na pia swala ya Ijumaa kila wiki, wao huwazuru wagonjwa, huwenda mazikoni, wanakwenda hajj baada ya hajj, na juu ya hayo yote wao hupigana katika njia ya Allah (s.w). Wanapokwenda Hajj au katika Jihad, sisi huwatunzia mali zao tukawalea watoto wao na tukawashonea nguo zao. Je nasi hatupati sehemu katika thawabu zao?"*

Mtume SAAW aliwaelekea Maswahaba waliokuwa pamoja naye, akasema: *Jee mumewahi kumsikia mwanamke akiuliza swali bora kuliko hili ?"*

Maswahaba ra. walimjibu:

*"Ewe, Rasulullahi! Hatukufikiria kamwe kuwa anaweza kuuliza swali kama hili."*

Mtume SAAW akwambia Asma :

*"Sikiza kwa makini halafu nenda ukawaambie kwa wenzako wanawake waliokutuma, mwanamke akitafuta radhi za mumewe, na akazitekeleza kazi za nyumbani kwake mpaka mumewe akaridhika, anapata malipo sawa sawa na mume kwa ibada zote anazozifanya huyo mume."*

Nasaha hizi za Mtume SAAW ziondoshe hisia za unyonge wa akinamama juu ya uhafifu wa amali zao hususan ndani ya mwezi huu wa Ramadhani. Aidha, nasaha hizi zisiwe kisingizio cha wanaume kuwatwisha makazi mengi wake zao kiasi cha kuwakosesha fursa kujihusisha na ibada kwa kadiri inavyowezekana.

Tunamuomba Allah SWT Katika mwezi huu mtukufu Atuokoe na moto na ahli zetu na Atuingize katika Pepo kwa Rehma zake , tuwe pamoja na wema waliotangulia na Mashahidi - Amiin

Iran kumiliki silaha za nyuklia wala kuendeleza uwezo wa makombora ya masafa marefu.

Waziri Mkuu wa Israel, Benjamin Netanyahu, aliunga mkono msimamo huo, akifuatilia nyayo za mshirika wake kwa kauli zenye msisitizo mkali kuhusu "usalama wa Israel" na kuzuia kile alichokiita tishio la Iran.

Kwa upande wake, Waziri wa Mambo ya Nje wa Iran, Abbas Araghchi, alitangaza kuwa Iran itatumia uwezo wake wote wa kijeshi kujilinda, akisisitiza kuwa ni haki ya kiasili na ya kisheria ya taifa lake kujitetea dhidi ya uchokozi (Al Jazeera, 28/02/2026). Iran nayo ilijibu kwa kurusha makombora kuelekea maeneo ya kijeshi ya dola ya Kiyahudi na kambi za Marekani katika eneo la Ghuba.

Hivyo, ndege za kivita za dola ya Kiyahudi na zile za Marekani, zikifanya operesheni kutoka nchi kavu, baharini na angani, zilishambulia kambi za kijeshi, vituo vya serikali na miundombinu inayodaiwa kuhusiana na mpango wa nyuklia wa Iran.

Mashambulizi mengi yalilenga mji mkuu pamoja na makao makuu ya taasisi za dola, ikiwemo ofisi za juu za uongozi wa kisiasa. Kauli za awali kutoka vyanzo vya kijeshi zilieleza kuwa mashambulizi hayo yanaweza kuendelea kwa muda wa siku nne hadi kumi, na huenda yakawa operesheni ya wazi hadi kufanikisha lengo la kuiondolea Iran uwezo wa nyuklia na makombora ya kimkakati.

Kwa mujibu wa ripoti za Al Arabiya (28/02/2026), vyanzo vya Israel vilidokeza kuwa awamu ya kwanza ya mashambulizi inaweza kudumu takribani siku nne, vikiyataja kuwa ni mwendelezo wa vita vilivyoanza majira ya kiangazi Julai 2025. Chanzo cha Marekani kilinukuliwa kikisema kuwa kampeni ya sasa ya kijeshi inaweza kuendelea kwa takribani siku kumi, kulingana na tathmini ya hali ya operesheni.

Enyi Waislamu:

Shambulio hili limefanywa dhidi ya Iran katika hali ambayo kwa miaka mingi imekuwa ikizunguka katika mhimili wa ushawishi wa Marekani. Iliwahi kutoa mchango wake katika mazingira ya vita vya Marekani dhidi ya Iraq na Afghanistan, pamoja na kushiriki katika mizania ya kisiasa ya eneo kwa namna iliyolinda maslahi ya kimkakati ya Washington. Katika kipindi hicho, Marekani haikuyapa uzito mkubwa masuala ya makombora na nyuklia kama inavyofanya leo; bali katika utawala wa Rais Barack Obama, yalifikiwa makubaliano ya mwaka 2015 (JCPOA) kwa ushirikiano wa nchi za Ulaya, yaliyomruhusu Iran kurutubisha urani kwa kiwango cha asilimia 3.67 chini ya uangalizi wa kimataifa.

Iran iliendelea kubaki katika mwelekeo huo kwa miaka kadhaa. Hata hivyo, alipoingia madarakani Donald Trump, alijiondoa katika makubaliano hayo na kuanza sera ya shinikizo kali, akitaka Iran ibadilishe mwenendo wake wa kisiasa na kimkakati. Mazungumzo yaliendeshwa katika mji wa Muscat kwa duru kadhaa, yakafuatiwa na mashambulizi yaliyoitwa "mashambulizi ya siku kumi na mbili".

Kwa mujibu wa BBC (22/06/2025), Trump alitangaza kulenga vituo vitatu vya nyuklia vya Iran Fordow, Natanz na Isfahan akidai kuwa operesheni hiyo imefanikiwa, na akaitaka Iran kukubali masharti ya amani kwa mtazamo wa Marekani.

Hata hivyo, mashambulizi hayo hayakufanikisha kuibadilisha Iran kutoka dola inayojaribu kuhifadhi uhuru wake wa kisiasa kuwa dola tegemezi inayofuata maelekezo ya nje. Badala yake, sauti za ndani zilianza kujitokeza zikikosoa utegemezi wa kimkakati na kuhimiza kujinasua katika mivutano ya kimataifa. Marekani ilirejea tena katika mkondo wa mazungumzo, lakini kwa misingi ile ile ya kudai kuondolewa kwa uwezo wa makombora na nyuklia wa Iran. Kama ilivyotokea awali, duru za mazungumzo zilifuatwa tena na mashambulizi.

Enyi Waislamu:

Hakika watawala katika nchi za Waislamu hawajatambua hatari ya kuifanya mustakabali wa mataifa yao utegemee ridhaa ya dola za kikafiri. Uzoefu wa kihistoria unaonyesha kuwa dola za kikafiri hutanguliza maslahi yao pekee, na hazisiti kuachana na washirika wao pale wanapoona manufaa yao yamebadilika. Mara nyingi,

**Inaendelea uk ...7**

# MTAZAMO JUU UUZWAJI WA AKIBA YA DHAHABU YA TANZANIA

Benki Kuu ya Tanzania (BoT) hivi karibuni imefafanua kuwa inapanga kuuza sehemu akiba ya dhahabu ili kudhibiti ukwasi na kukabiliana na athari na misukosuko ya kiuchumi inayoweza kutokea hasa kutoka nje ya nchi, hatua ambayo imezua mjadala mkubwa miongoni mwa Umma.

Kwa mujibu wa Benki Kuu ya Tanzania (BoT) thamani ya akiba ya dhahabu iliyokusanywa kwa sasa ni dola za Marekani bilioni 3.24, wakati lengo likiwa ni kukusanya akiba ya thamani ya dola bilioni 2, hivyo kuna ziada ya dola bilioni 1.2. Akiba ya fedha za kigeni kwa sasa ni takribani dola bilioni 6.52, ambapo dhahabu inachangia dola bilioni 1.2, dola za Marekani ni bilioni 3.8, na Yuan ya China ni dola milioni 735.

Hapana shaka BoT inauza sehemu ya akiba ya dhahabu ili kupata dola za Marekani kwa ajili ya kusimamia uagizaji wa bidhaa kutoka nje. Kiasi cha akiba ya pesa za kigeni kilichopo sasa cha dola bilioni 6.52 kinatosha kugharamia takribani miezi 4.9 tu ya uagizaji.

Uamuzi huu wa BoT unaonesha ukweli mchungu katika namna mbili :

Kwanza, ni namna gani uchumi wa dunia hususan mataifa yanayoendelea, unavyotegemea kwa kiasi kikubwa dola ya Marekani katika miamala yao ya kiuchumi na kifedha. Jambo hili ni ajenda ya uchumi wa kinyonyaji wa kikoloni iliyoasisiwa na Marekani tangu Makubaliano ya Bretton Woods ya



mwaka 1944. Makubaliano hayo yalileta athari kuu mbili:

A. Kutupiliwa mbali kwa mfumo wa fedha unaotegemea dhahabu (gold standard) na kuhamia kwenye mfumo wa fedha za karatasi (paper standard), ambao umekuwa ukisababisha kuyumba na misukosuko ya kiuchumi na kifedha.
B. Kuimarishwa kwa nafasi ya Marekani kwa kuipa uwezo na mamlaka ya kuathiri na kudhibiti uchumi wa dunia kupitia sarafu yake kama sarafu yenye nguvu zaidi kimataifa.

Nchi za kikoloni za kimagharibi na hasa Marekani hutumia sarafu zao kama chombo cha kudhibiti na kuathiri mataifa dhaifu kiuchumi na kisiasa. Inasikitisha sana kuona kwamba mataifa maskini yanayoendelea hulazimika kuuza akiba yao ya dhahabu ili kupata fedha za karatasi kwa ajili ya kusimamia uagizaji wa bidhaa. Kwa kuwa Marekani kwa sasa ndio taifa linaloongoza na kinara wa mfumo wa kibepari hufanya kila jitihada kulinda hali hii kwa maslahi yake na huitumia hali hiyo kutilia nguvu katika kulinda na kuhifadhi mfumo wake muovu wa kinyonyaji kupitia ubabe wa sarafu yake na kuubena uchumi wa kilimwengu kwa maslahi yake.

Pili, katika jambo hili kwa kiasi kikubwa kunadhihirika wazi kwamba kiasi cha dhahabu ilichonacho BoT bado ni kidogo mno, hasa ikizingatiwa kuwa Tanzania ni miongoni mwa wazalishaji wakubwa wa dhahabu.

Ingawaje hatupingi uwepo wa mfumo wa rushwa ya ndani ya nchi, lakini hilo ni sehemu tu, bali hoja msingi hapa ni kwamba Tanzania kama yalivyo mataifa mengi yanayoendelea, haimiliki kikamilifu rasilimali zake za dhahabu. Badala yake, humilikiwa na kudhibitiwa na makampuni makubwa ya kikoloni ya kinyonyaji ya kimataifa ya mataifa makubwa chini ya mwamvuli wa uwekezaji wa kigeni. Hivyo, licha ya kutambulika kama mzalishaji mkubwa wa dhahabu, bado taifa linakabiliwa na umasikini mkubwa.

Kwa mujibu wa mfumo wa uchumi wa Kiislamu, sarafu inapaswa kuwa na thamani halisi ya dhahabu badala ya fedha za karatasi kama ilivyo leo chini ya ushawishi, nguvu na ukoloni wa Marekani. Hilo la sarafu kuwa ya thamani ya dhahabu huleta uthabiti wa uchumi na kuzuia kuyumbayumba na kuporomoka kwa mifumo ya kifedha.

Aidha, Uislamu upo mbali na mfumo wa uchumi wa kibepari ambao kwa makusudi huinyonga dhana ya umiliki kwa maslahi yake. Uislamu unaainisha wazi aina za umiliki: umiliki wa dola (serikali), umiliki binafsi na umiliki wa Umma ambapo kiasi kikubwa cha maadini

**Inaendelea uk...7**

## Mashambulizi Iran … kutoka uk 5

urafiki wao ni wa muda na wa kimkakati; hujenga mahusiano kwa manufaa ya muda mfupi na kuyaachilia pindi wanapopata wanachotaka.

Lau watawala hawa wangechukua mazingatio ya historia ya siasa za kimataifa, wangeona namna mawakala na washirika wa muda walivyoachwa au hata kuondolewa baada ya kutimiza majukumu yao. Hata hivyo, hali ya utegemezi imefikia kiwango kwamba nchi inaposhambuliwa, nyingine hubakia watazamaji, zikitoa matamko yasiyo na athari au kuhesabu idadi ya wahanga bila kuchukua hatua za kulinda hadhi na usalama wa eneo lao.

Enyi Waislamu:

Hakika heshima na nguvu ya Umma imo katika kurejea kwa uongozi wake wa kisiasa unaotokana na itikadi yake. Hizb ut Tahrir inatangaza kuwa imejitolea kufanya kazi kwa bidii na kwa ikhlasi ili kurejesha maisha ya Kiislamu kwa kusimamisha tena Khilafah Rashidah kwa mujibu wa njia ya Utume. Inajitazama kama chama cha kisiasa chenye mradi wa kimfumo, kinacholenga kuunganisha Umma chini ya uongozi mmoja wa Kiislamu, kwa misingi ya Qur'an na Sunnah.

Kwa mujibu wa mtazamo huu, kurejea kwa Khilafah kungekuwa ni hatua ya kuimarisha umoja wa Waislamu, kulinda ardhi na rasilimali zao, na kurejesha mizania ya nguvu katika medani ya kimataifa. Hivyo ndivyo wanavyoliona kuwa suluhisho la msingi la kuondoa hali ya udhaifu wa sasa na kuzuia maadui kuthubutu kuivamia ardhi ya Waislamu bila hofu ya madhara makubwa.

Ama dola ya Kiyahudi, kwa mtazamo huu wa kisiasa, hudumu kwa msaada wa nje na uungwaji mkono wa kimkakati kutoka Marekani na baadhi ya mataifa ya Ulaya. Msingi wa nguvu yake haujajengwa katika uwezo wa kujisimamia pekee, bali katika miungano ya kijeshi na kiusalama.

Tatizo kubwa, kwa mtazamo huu, haliko tu katika mashambulizi ya nje, bali katika hali ya mgawanyiko na utegemezi ndani ya nchi za Waislamu. Watawala wanaochagua kufuata sera za mataifa ya kikafiri kwa gharama ya maslahi ya Umma wao huendeleza udhaifu wa kisiasa na kijeshi. Badala ya kusimamisha hukumu za Mwenyezi Mungu na kuunganisha safu za Umma, wanabaki katika mifumo inayotawaliwa na maamuzi ya nje.

Kwa hiyo, mabadiliko ya kweli kwa mujibu wa mtazamo huu yanahitaji kurejea katika misingi ya Kiislamu ya uongozi, kusimamisha utawala unaojitegemea, na kuunganisha nguvu za Umma ili Uislamu na Waislamu wapate izza, na dhulma na uonevu vikomeshwe.

11 Ramadhani 1447H

Jumamosi, 28 Februari 2026

Hizb ut Tahrir

******************

## Akiba ya dhahabu..kutoka uk 6

kama dhahabu huwa ni mali ya Umma. Pia mali za Umma huhusisha huduma zote muhimu ambazo kukosekanwa kwake jamii hulazimika kutawanyika kuzitafuta, kama vile vyanzo vya maji, malisho ya mifugo na mfano wake.

Ubepari umeubagwa chini ulimwengu katika nyanja zote za maisha, unazua vurumai katika siasa, unasambaratisha maadili ya kijamii na umeneza unyonyaji wa kiuchumi kila mahala. Ni jukumu la watu kupokea mfumo mbadala wa Uislamu ulio na masuluhisho thabiti na ya kiwahyi kwa matatizo yote ya mwanadamu.

Imeandikwa na Said Bitomwa
Mjumbe wa Afisi ya Habari ya
Hizb ut Tahrir Tanzania
Kwa Afisi Kuu ya Habari ya
Hizb ut Tahrir

********

## Upasuaji. kutoka uk .4

Ushahidi wa hilo ni alivyosimulia al-Bukhari kupitia Alqama, alisema:*"Mwenyezi Mungu amewalaani wanawake wanaojichora tattoo (Washimat) na wanawake (Mustawshimat) walio kata nywele za uso na nyusi (Mutanammisath), na wanawake wanaotenganisha meno yao ya mbele kwa kujirembesha, wanao badilisha aliyoumba Mwenyezi Mungu."*

**Ndugu yenu**
**Sheikh Ataa bin Khalil**
**Amiri wa Hizb ut Tahrir**

# MASHAMBULIZI YA MAREKANI NA ISRAEL KWA IRAN :

Wanaharakati wa Hizb ut Tahrir Tanzania mara baada ya Ijuma ya tarehe 6 Machi 2026 wakifanya visimamo vya mabango sehemu mbalimbali kulaani mashambulizi ya Marekani kwa Iran na kuyataka majeshi katika ulimwengu wa Kiislamu kuungana kumfukuza adui





















